

# Notisi ya Karo ya Shule kwa Familia za Wanafunzi wa Gredi K-6



## Katiba ya Utah hairuhusu karo kwa watoto wa shule za kimsingi.

Watoto wa chekechea hadi gredi ya 6 hawataitishwa vitabu, vifaa vya matumizi darasani, ala za muziki, safari za nje, mkusanyiko, vitafunio (kando na chakula kinachotolewa Katika mpango wa chakula Shuleni), ama kwa kitu kingine chochote kinachofanyika ama kutumika Katika siku za kawaida Shuleni.

**Karo yaweza tu kuitishwa kwa** mipango inayofanyika kabla ama baada ya shule, ama baada ya shule kufungwa. Karo yaweza pia kuitishwa kwa mwanafunzi aliye katika gredi ya sita katika shule ambayo pia inahusisha moja au zaidi ya gredi 7-12, kama shule hiyo inafuata mtindo wa sekondari wa kutoa Elimu kwa wanafunzi wa gredi ya sita.

Sheria ya Utah inazihitaji shule zinazoitisha karo, kuhakikisha ya kuwa ondoleo la karo ama mahitaji mengine yanatolewa kwa mwanafunzi yeyote ambaye wazazi wake hawana uwezo wa kulipa karo.

## Ondoleo la Karo

Ondoleo la Karo ni kutohitajika kulipa karo. Kama mwanafunzi anasitahili ondoleo la Karo, **karo yote lazima iondolewe**. Kama haijatajwa na kushughulikiwa ipasavyo katika Sheria ya Jimbo, lazima shule iondoe karo yote, ikiwemo popote mwanafunzi anahitajika kushiriki kwa hiari. Hii inamaanisha kuwa wanafunzi wote wanaositahili ondoleo la Karo wanaweza kushiriki darasa lolote ama shughuli shuleni bila kulipishwa chochote.

Mwanafunzi anahitimu ondoleo la karo kama:

- familia ya mwanafunzi hupokea hela za TANF (food stamps ama mpango wa Family Employment Program);
- mwanafunzi hupokea SSI (Supplemental Security Income);
- mwanafunzi ametajwa kama McKinney-Vento;
- mwanafunzi anapokea malezi yasiyo ya familia halisi;
- mwanafunzi anapokea malezi ya serikali;
- mwanafunzi anahitimu kufuatana na mapato ya familia yake (Viwango vinatoshana na vile vinavyohitajika ili kuhitimu kupokea chakula cha bure).

*\* Mwanafunzi anaweza pia kuhitimu kupokea ondoleo la karo Hata asipoweza kufikia mahitaji haya, lakini awe bado hana uwezo wa kulipa karo. Tafadhali tazama taratibu za shule ama wilaya kwa maelezo zaidi.*

Kama mwanafunzi anataka kutuma ombi la ondoleo la karo, ataitishwa stakabadhi za kuonyesha ya kwamba anahitimu ondoleo la karo. Hii ni sehemu ya utaratibu wa kuthibitishwa.

Ili kutuma ombi la ondoleo la karo, mwanafunzi atajaza fomu ya “Fee Waiver Application (Gredi K-6)”. Nakala ya fomu ya ombi hili inapatikana katika notisi hii. Nakala zaidi zinapatikana ofisini Shuleni, ama kwenye Tovuti ya karo katika Jimbo, iliyoko mwishoni mwa stakabadhi hii. Punde tu baada ya stakabadhi kuwasilishwa shuleni, hitaji la kulipa karo litasimamishwa hadi uamuzi mwafaka utakapoafikiwa kuhusu ombi la mwanafunzi la ondoleo la karo..

Kama ombi litakataliwa, shule itatuma fomu ya “Decision and Appeal Form”. Fomu hii inaeleza sababu ya ombi kukataliwa na jinsi ya kupinga uamuzi huo. Kumbuka kila wakati kujiwekea nakala yako. Kama rufaa dhidi ya kukataliwa kwa ombi la ondoleo la karo itawasilishwa hakuna karo itakayolipwa hadi rufaa hiyo iamuliwe.

Mwanafunzi akitaka kununua picha shuleni, yearbooks, ama vitu vingine kama hivyo shuleni, hiyo gharama si karo, wala haitaondolewa. Pia, mwanafunzi akipoteza ama akiharibu mali ya Shule, gharama ya kurejesha ama kurekebisha si karo, wala haitaondolewa.



## Michango, Usiri, na Utekelezaji wa Malipo ya Karo

Pesa shuleni ni kidogo, na shule yaweza kuhitaji msaada, kando na karo. Kwa hivyo, shule yaweza kuomba michango inayotowza ushuru, ya mahitaji shuleni, vifaa, ama pesa, lakini haiwezi ikaitisha ama kuhitaji kufanyiwa mchango.

Shule na wafanyikazi shuleni hawawezi kuzuia, kupunguza ama kuongeza gredi, ama kuzuilia gredi, taratibu za shughuli darasani, kadi ya ripoti, karatazi za mitihani, ama diploma ili kuhimiza malipo ya karo.

**Kwa Maelezo Zaidi, wasiliana na:** \_\_\_\_\_

### Shule:

Jina: \_\_\_\_\_ Simu: \_\_\_\_\_

Email: \_\_\_\_\_ Tovuti: \_\_\_\_\_

### Anwani ya Msimamizi wa Maswala ya Karo Wilayani/Charter School:

Jina: \_\_\_\_\_ Simu: \_\_\_\_\_

Email: \_\_\_\_\_ Tovuti: \_\_\_\_\_

Tovuti ya karo, ya Bodi ya Elimu Katika Jimbo la Utah <https://schools.utah.gov/schoolfees>